# TUZO ZA MWANAWETUBOOKS

Mwanawetu Books & Consultancy

M B & C

© 2022

# SHINDANO LA UANDISHI WA HADITHI FUPI

## KWA

## WANAFUNZI WA SHULE ZA SEKONDARI

## LINDI, MTWARA, NA RUVUMA

 © 2022

# YALIYOMO

1.0 UTANGULIZI ........ 4
1.1 LENGO LA SHINDANO ........ 4
1.2 MADA ........ 4
2.0 MAELEZO KUHUSU SHINDANO ........ 5
2.1 JINSI YA KUTUMA IKISIRI ........ 5
2.2 Tuzo ........ 5
2.3 SIRI YA USHINDI ........ 5
3.0 UTEKELEZAJI WA MRADI ........ 6
4.0 MATOKEO ........ 7
4.1 MATOKEO YA SHINDANO LA UANDISHI WA HADITHI FUPI KWA WANAFUNZI WA SHULE ZA SEKONDARI KANDA YA KUSINI MWAKA 2022 ........ 7
4.2 HADITHI ZILIZOKIDHI VIGEZO VYA SHINDANO LA UANDISHI WA HADITHI FUPI KWA WANAFUNZI WA SHULE ZA SEKONDARI ........ 8
5.0 TATHIMINI ........ 9
5.1 MAELEZO KUHUSU WASHINDI ........ 9
5.2 TATHMINI KUHUSU MRADI ........ 10
6.0 HADITHI ........ 11
6.1 HADITHI YA MSHINDI WA KWANZA ........ 11
........ 14
6.2 HADITHI YA MSHINDI WA PILI ........ 14
6.3 HADITHI YA MSHINDI WA TATU ........ 18
6. 4 HADITHI YA MSHINDI KATI YA WASHINDI KUMI (10) ........ 19
6.5 ZAWADI ........ 19

 © 2022

# 1.0 UTANGULIZI

Mwanawetu Books and Consultancy (MBC) ni Maktaba ya digitali nchini Tanzania. Imesajiliwa na Brela kwa namba 502151 mwaka 2021, BASATA mwaka 2021, COSOTA namba ya uanachama A085926, TRA –TIN 122-509-893, na namba ya utambulisho Maktaba ya Taifa ni 5713.

Lengo kuu la maktaba hii ni kuenzi na kuiendeleza lugha ya Kiswahili. Katika kutimiza lengo hilo, MBC imeshirikisha Wanafunzi wa ngazi ya Shule za Sekondari kufanyia kazi mada walizosoma wakiwa shuleni kuhusu Fasihi Simulizi na Fasihi Andishi.

## 1.1 LENGO LA SHINDANO

- Kwenda sambamba na utekelezaji wa mpango mkakati wa sasa wa Wizara ya Elimu unaohitaji wanafunzi kupimwa kiwango cha uelewa kwa kutumia "Comptence Based Assessment" badala ya "Content Based Assessment". Hivyo kupitia utungaji wa hadithi itaonesha uelewa/ujuzi wa mwanafunzi alioupata baada ya kujifunza kazi mbalimbali za sanaa na vipera vyake.
- Kukuza lugha ya Kiswahili
- Kuibua vipaji vya utunzi na uandishi wa hadithi na vitabu
- Kushirikisha wanafunzi katika kuielezea jamii inayowazunguka.
- Kuwajengea uwezo na ujasiri (wanafunzi/watoto) wa kueleza mambo wanayoyafahamu kuhusu jamii
- Kuwapa uwanja wa kueleza changamoto au mafanikio ya jamii
- Kuwasilisha kazi za Sanaa
- Kuhamasisha shughuli nyingine ya kiuchumi (madini) tofauti na zile zilizozoeleka na wakazi wa mikoa hiyo ambazo ni kilimo, uvuvi, ufugaji, na biashara kwa njia ya sanaa.

### 1.2 MADA

Inatokana na kauli mbiu ya Siku ya Wanawake Duniani 2022 "SERIKALI YETU MADINI YETU" ambayo imetumika na taasisi zilizopo Kanda ya Ziwa.

### *1.2.1 Kwanini kauli mbiu "Serikali yetu, madini yetu" itumike Kanda ya Kusini?*

Maeneo mengi ya Kanda ya Kusini yanaonekana kuwa na migodi mingi ya madini mbalimbali. Migodi hiyo imeweza kunufaisha jamii nyingi za Kitanzania na nje ya nchi. Mfano wa migodi hiyo ni mgodi wa shaba ya bluu Tunduru mkoani Ruvuma, makaa ya mawe wilayani Mbinga, Nyasa. Pia mkoani Lindi kuna migodi ya mawe ya gypsum wilayani Kilwa, gesi asilia Songosongo wilayani Kilwa na mgodi wa dhahabu na green tomalin wilayani Ruangwa. Wakati mkoani Mtwara ikiongozwa na uchimbaji mkubwa wa gesi asilia na uzalishaji wa chumvi na chokaa.

Kuhusianisha madini na wanawake wa Ukanda wa Kusini kumelenga kuweka bayana mafanikio au changamoto zinazowakabili wanawake na wasichana katika ushiriki/ushirikishwaji wa kazi za migodini.

## 2.0 MAELEZO KUHUSU SHINDANO

MBC inawakaribisha Wanafunzi wote wa Shule za Sekondari zilizopo katika mikoa ya Lindi, Mtwara, na Ruvuma; kushiriki katika shindano hili la Uandishi wa hadithi fupi.

Hadithi ziwe na maneno yasiyopungua mia mbili hamsini (250). Ziandikwe kwa mkono au kuchwapwa kwa mashine (kompyuta). Michoro inaruhusiwa.

### 2.1 JINSI YA KUTUMA IKISIRI

Ili kurahisisha mawasiliano; hadithi zote zitumwe zikiwa zina jina la Mwandishi (Mwanafunzi), jina la Shule anayosoma Mwandishi, kidato, namba za simu za Walimu wa Shule husika. Ni vema hadithi zikipitia kwenye ofisi ya uongozi wa Shule au idara ya lugha ya Kiswahili ya Shule husika.

Hadithi zitumwe kupitia baruapepe info@mwanawetubooks.co.tz au WhatsApp 0737 966996 kuanzia tarehe 14 Februari, 2022 na mwisho wa kupokea hadithi ni tarehe 28 Februari, 2022.

### 2.2 Tuzo

Mshindi wa kwanza atapata zawadi ya cheti, fedha taslimu Tsh. 100,000/= pamoja na vifaa vya shule wakati washindi wengine 10 watapata zawadi mbalimbali pamoja na fedha taslimu.

Hadithi 10 bora zitachapishwa kwenye maktaba ya kidigitali inayopatikana mtandaoni kupitia tovuti; https://www.mwanawetubooks.co.tz

Washindi wote watatangazwa tarehe 28 Machi, 2022, katika sherehe ya maadhimisho ya Juma la Elimu mkoa wa Mtwara.

### 2.3 SIRI YA USHINDI

- Uwezo wa kuhusianisha lugha ya Kiswahili, wahusika, na mada iliyotolewa.
- Matumizi ya visawe visivyotumika mara kwa mara na Wazungumzaji wa lugha ya Kiswahili nchini Tanzania
- Mtiririko na mpangilio wa visa na wahusika
- *Matumizi mazuri ya lugha ya Kiswahili*
- *Uwezo wa kuhusianisha migodi/madini na maisha halisi ya wanawake waishio mikoa ya Lindi, Mtwara, na Ruvuma*
- *Mwandishi awe mwanafunzi wa Shule za Sekondari zilizomo ndani ya mikoa ya Lindi, Mtwara, na Ruvuma*

*Kwa mawasiliano zaidi, wasiliana nasi kupitia*;
Namba ya simu ya mkononi; 0737966996
Baruapepe; info@mwanawetubooks.co.tz

## 3.0 UTEKELEZAJI WA MRADI

Shindano hili la uandishi wa hadithi fupi litakamilika katika kipindi cha miezi mtatu kuanzia mwezi Februari hadi Aprili 2022

| Na. | Shughuli ya kutekelezwa | Muda wa utekelezaji | Mahali | Wahusika |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Maandalizi ya mashindano; Andiko la mradi | 1ST na 3rd | Mtwara | MBC |
| 2. | Vibali | Wiki ya 3, Februari | Lindi, Mtwara, Ruvuma | RAS |
| 3. | Matangazo ya radio;<br>HFM<br>Kipindi cha redio, radio Safari<br>Mitandao ya kijamii; facebook na instagram<br>Website | Kuanzia tarehe 14/2/2022<br>Hadi 28/2/2022 | Mtwara, Ruvuma, na Lindi<br><br>Mtandaoni | MBC |
| 4. | Kupokea hadithi toka shule mbalimbali | 17/2/2022 hadi 28/2/2022 | Email; info@mwanawetubooks.co.tz<br><br>WhatsApp Namba **0737966996** | MBC |
| 5. | Zoezi la kumtafuta mshindi | Tarehe 3/3/2022 hadi 5/3/2022 | Walimu wa lugha ya Kiswahili | MBC |
| 6. | Kutangaza Washindi | 7/3/2022 | | MBC |
| 7. | TUZO | 28/3/2022 hadi 2/4/2022 | Kamati | Kamati na MBC |

 © 2022

## 4.0 MATOKEO

4.1 MATOKEO YA SHINDANO LA UANDISHI WA HADITHI FUPI KWA WANAFUNZI WA SHULE ZA SEKONDARI KANDA YA KUSINI MWAKA 2022

**WASHINDI KUMI (10)**

| Na | JINA | JINSI | KIDATO | SHULE | WILAYA | MKOA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Omary Hassan Makunganya | ME | III Ujenzi | Mtwara Tech | Mtwara | Mtwara |
| 2. | Hussein Abdallah Hussein | ME | IV Mitambo | Mtwara Tech. s.s | Mtwara | Mtwara |
| 3. | Hawa Salumu Mgaya | KE | I | Nasuli s.s | Namtumbo | Ruvuma |
| 4. | Sadat Jamali Malunda | ME | III | Mikindani s.s | Mtwara | Mtwara |
| 5. | Jackline Stephen Mpunga | KE | II | Mtapika s.s | Masasi | Mtwara |
| 6. | Rukia Ahmad Mpinga | KE | III | Milola s.s | Lindi | Lindi |
| 7. | Ariel Queen John | KE | III Mitambo | Mtwara Tech | Mtwara | Mtwara |
| 8. | Sauda Twalibu Ramadhani | KE | IV Mitambo | Mtwara Tech.s.s | Mtwara | Mtwara |
| 9. | Sabrina Amani Maluzuku | KE | IV | Mtapika s.s | Masasi | Mtwara |
| 10 | Scholastica Benjamin Luambano | KE | III Mitambo | Mtwara Tech.s.s | Mtwara | Mtwara |

4.2 HADITHI ZILIZOKIDHI VIGEZO VYA SHINDANO LA UANDISHI WA HADITHI FUPI KWA WANAFUNZI WA SHULE ZA SEKONDARI

**HADITHI ILIYOANDIKWA NA;**

| Na. | JINA | JINSI | KIDATO | SHULE | WILAYA | MKOA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Sabrina Amani Maluzuku | KE | IV | Mtapika s.s | Masasi | Mtwara |
| 2. | Seleman Mussa Hassan | ME | I | Mtapika s.s | Masasi | Mtwara |
| 3. | Jackline Stephen Mpunga | KE | II | Mtapika s.s | Masasi | Mtwara |
| 4. | Sadat Jamali Malunda | ME | III | Mikindani s.s | Mtwara | Mtwara |
| 5. | Muksini Ally | ME | III | Mikindani s.s | Mtwara | Mtwara |
| 6. | Rukia Mpinga | KE | III | Milola s.s | Lindi | Lindi |
| 7. | Hawa Salumu | KE | I | Nasuli s.s | Namtumbo | Ruvuma |
| 8. | Charity David Wilson | KE | I | Mtwara Ufundi s.s | Mtwara | Mtwara |
| 9. | Faisal Bashiri Nachuli | ME | IB | Mtwara Ufundi s.s | Mtwara | Mtwara |
| 10. | David Waziri Myovele | ME | I | Mtwara Ufundi s.s | Mtwara | Mtwara |
| 11. | Scholastica Benjamin Luambano | KE | III Mitambo | Mtwara Ufundi s.s | Mtwara | Mtwara |
| 12. | Ariel Queen John | KE | III Mitambo | Mtwara Ufundi s.s | Mtwara | Mtwara |
| 13. | Abuidhwaifa Hamidu Haridi | ME | III | Mtwara Ufundi s.s | Mtwara | Mtwara |
| 14. | Yasini Shaibu Kachewa | ME | III Umeme | Mtwara Ufundi s.s | Mtwara | Mtwara |
| 15. | Hussein Abdallah Hussein | ME | IV | Mtwara Ufundi s.s | Mtwara | Mtwara |
| 16. | Omary Hassan Makunganya | ME | III CIVIL | Mtwara Ufundi s.s | Mtwara | Mtwara |
| 17. | Mohamed Salim Pengo | ME | IB | Mtwara Ufundi s.s | Mtwara | Mtwara |
| 18. | Sauda Twalibu Ramadhani | KE | IV Mechanical | Mtwara Ufundi s.s | Mtwara | Mtwara |
| 19. | Ikram Kassim Mlekeni | ME | I | Mtwara Ufundi s.s | Mtwara | Mtwara |
| 20. | Praynod Jacob Mahela | ME | IC | Mtwara Ufundi s.s | Mtwara | Mtwara |


© 2022

# 5.0 TATHIMINI

## 5.1 MAELEZO KUHUSU WASHINDI

**Mshindi wa kwanza;**

Hadithi hii imepata hadhi ya kuwa ya kwanza katika shindano hili kwa kuwa imegusa changamoto wanazopitia wanawake katika jamii nyingi za wakazi wa mikoa ya Lindi, Mtwara, na Ruvuma kama ifuatavyo;

Mtunzi **Omari H. Mkunganya** Kidato cha III Ujenzi, katika Shule ya Sekondari Mtwara Ufundi; ameeleza jinsi Mzee Makunganya alivyokuwa anampiga mkewe kisa hana mtoto wa kiume. Kipindi ambacho jamii yao ilithamini watoto wa kiume na kudharau watoto wa kike na wanawake kwa ujumla. Pia ameeleza manyanyaso aliyopitia mke wa Mzee Makunganya aliyekuwa ananyang'anywa ujira wake aliuopata baada ya kufanyakazi kwenye migodi ya chumvi. Mume alikuwa anachukua na kuzitumia fedha hizo za mkewe, kununulia pombe za kienyeji (mataputapu).

Kwa upande wa suluhisho la migogoro, mtunzi ameeleza jinsi uchaguzi wa Serikali za Mitaa uliozingatia usawa wa kijinsia, huru, na haki kwa wote unavyoweza kuvunja mila potofu na kuleta amani kwenye jamii.

Mtunzi wa hadithi hii ametumia ubunifu wa kutamba hadithi kwa mtindo wa ushairi. Hivyo kuifanya hadithi iwe na msisimko wa kipekee.

**Mshindi wa pili;**
Mtunzi wa hadithi hii; **Hussein Abdallah Hussein**, kidato cha Nne Mitambo, Shule ya Sekondari Mtwara Ufundi; ameeleza umuhimu wa kutia bidii binafsi katika kila jambo ili kufikia maendeleo.

Pia ameeleza kuhusu ukombozi wa mwanamke/wasichana kutoka kwenye mila potofu. Imejidhihirisha pale Samia aliponyimwa fursa ya kwenda shule wakati kaka zake walipelekwa. Samia alionesha kujikomboa pale alipoamua kujifunza kusoma na kuandika kwa kutumia mfumo usio rasmi.
Matumizi sahihi ya vyombo vya habari pale Samia alipopata taarifa ya ajira kupitia tangazo la kwenye gazeti.
Mwandishi ametumia hadithi na michoro ambayo inasaidia kuongeza ufafanuzi wa masimulizi yake.

**Mshindi wa tatu;**
Mtunzi wa hadithi hii ameeleza jinsi mwanawake alivyobeba jukumu la kutunza familia yenye watoto watatu peke yake baada ya mume wake kufariki (Single mother/parent). Pia ameeleza sababu zinazopelekea watoto /wanafunzi kuacha shule (droup-out) na kwenda kujiunga na shughuli mbalimbali (child labour) wakihisi ndiyo mbadala wa shule katika kufikia maendeleo. Imejidhihirisha pale John alipoacha shule na kwenda migodini kutafuta fursa za ajira lakini alishindwa kufikia malengo na kuamua kurudi tena shuleni.
Pia Mwandishi ameonesha kuwa wanafunzi wanaoacha shule kwa sababu mbalimbali, wanaweza kurudi shuleni kisha kufanya vizuri kama vile John alivyoweza kuajiriwa na Serikali baada ya kuhitimu masomo yake kwa awamu ya pili.

 © 2022

## 5.2 TATHMINI KUHUSU MRADI

### A) Kauli mbiu

Kauli mbiu iliyotumika katika shindano hili la uandishi wa hadithi fupi “Serikali yetu, madini yetu” ambayo ilitumiwa na Chama cha Wanawake wanunuzi wa madini nchini Tanzania katika maadhimisho ya siku ya wanawake Duniani wakiwa mkoani Geita.

Ikiwa madini ya aina mbalimbali yanachimbwa kote nchini Tanzania ikiwemo katika mikoa ya Kanda ya Kusini ni sawa, inawezekana ushiriki au ushirikishwaji wa wananchi ukawa tofauti.

Gesi asilia inapatikaka katika mikoa ya Lindi na Mtwara, kwa namna gani wanawake wanashiriki au kushirikishwa? Pia ushiriki wa wanawake katika migodi mingine iliyosambaa katika mikoa ya Kanda ya Kusini, upo kwa kiasi gani? Kuna vyama vinavyotetea wachimbaji/wanunuzi wa madini vilivyoundwa na kusimamiwa na wanawake wenyewe? Hamasa na elimu kuhusu kukuza uchumi kupitia madini, inatosha kwa upande wa wanawake na wasichana waishio katika Ukanda huo?

Kwa kutumia hadithi zilizotungwa na Wanafunzi wa shule za Sekondari mbalimbali zilizopo katika mikoa ya Kanda ya Kusini imeonesha ushiriki wa wanawake na wasichana katika shughuli mbalimbali za migodini, upo. Ingawa kwa kiasi kikubwa ushiriki wao umeegemea kwenye kuuza bidhaa na kutoa huduma mbalimbali za usaidizi. Pia migodi wanayojihusisha kikamilifu ni ile ya kuchimba mawe na kubonda kokoto pamoja na kuzoa chumvi.

Wanawake wengi wanaojishirikisha katika shughuli za kubonda kokoto au kuvuna chumvi wanatumia shughuli hiyo kama mbadala wa ajira kwa kaya zenye kipato duni, badala ya kazi yenye kuleta maendeleo binafsi na taifa kwa ujumla. Hali hii inaweza kuwafanya wanawake wanaoshiriki kwenye maeneo ya migodi kuendelea kuwa na maisha duni. Kwa kuwa wanaweza kukosa vigezo vitakavyowawezesha kupata mitaji kutoka serikalini au kwenye taasisi mbalimbali, zinazolenga kuendeleza sekta ya madini.

### B) Utunzi/Uandishi wa hadithi

Utunzi na Uandishi wa hadithi unategemea kipaji, kujua matumizi sahihi ya lugha husika (Kiswahili), uwezo mkubwa wa kutambua mambo mbalimbali yanayohusu utamaduni wa jamii husika (ili kujua upotofu au ukamilifu), uwezo wa kuchakata mambo yaliyofundishwa darasani au kuyaona kwenye mazingira yanayomzunguka kisha kutengenezea hoja/kisa na wahusika, uwezo wa kusimulia jambo kwa mtiririko sahihi, na uwezo wa kufanya tafakuri ya vitu halisi na dhahania.

Wanafunzi wa Shule za Sekondari zilizopo katika mikoa ya Lindi, Mtwara, na Ruvuma kupitia shindano hili la uandishi wa hadithi fupi zilizowasilishwa; imeonesha wanafunzi wana uwezo mkubwa katika kuwasilisha kazi za Fasihi simulizi na Fasihi Andishi. Vipaji vya kuchora hivyo ni rahisi kwao kutengeneza zana za kujifunzia kwenye masomo yao.

Alikadhalika, ufahamu wa matumizi sahihi ya lugha ya Kiswahili, na uwezo wa kuitambulisha lugha hiyo. Pia wameonesha uelewa mkubwa wa masomo wanayofundishwa darasani na kuweza kutekeleza wenyewe kile walichojifunza darasani bila kushurutishwa wala kusimamiwa.

Ingawa tangazo lilitolewa kwa muda mfupi, wanafunzi waliopata fursa ya kufahamu wito huo na kuwiwa kushiriki, wameweza kufanya vizuri. Hivyo hadithi zote ni nzuri na zinamafundisho makubwa kwa jamii inayowazunguka.

Wanafunzi wameonesha wana vitu vingi vichwani mwao; walivyofundishwa kwenye masomo au kujifunza kupitia mazingira ambavyo wanahitaji kuviwasilisha kwenye majukwaa mbalimbali.

# 6.0 HADITHI

## 6.1 HADITHI YA MSHINDI WA KWANZA

Hadithi! Hadithi!

Hapo zamani za kale, tena kale za mababu na mababu, kulikuwapo na kijiji kimoja kilichoitwa Patapata. Wakazi wa kijiji hicho walikuwa watu wema sana. Kijiji kilistawi na watu wema wakazidi kuzaliwa na kuongezeka. Ama kweli wakaongezeka watu wema, katika kijiji cha Patapata!

*Patapata ikasifika pande zote za dunia.*
*Kwa nje ikang’ara kwa vicheko vya wake wana.*
*Wengi waliutamani kuupata Upatapata,*
*ingawa wake Wana wakawa hatarini, vuruguni, na matatani.*
*Patapata ikajitia shidani, maendeleo yakawa hatarini.*
*Ingawa jamii ilikuzwa kwa yao mioyo,*
*wabeba wana walinyanyaswa, wakaonekana si watu.*

Katika kijiji hicho cha Patapata palikuwapo na mzee mmoja aliyeitwa Makunganya. Alikuwa na familia yenye watu wanne akiwemo mkewe pamoja na binti zake wawili ambao ni Akilinyingi na Adili. Siku zote mzee huyo alisikika akilalama huku akipiga kifua sehemu ya mtima, ya kwamba; kwanini hadi anazeeka hajafanikiwa kupata mtoto wa kiume?

Katika kijiji chao walikuwa na imani kuwa watoto wa kiume ndiyo wenye thamani kubwa katika familia zao. Kwa misingi hiyo, ikasababisha wabeba wana kuwekwa nyuma katika kila jambo, kuanzia masuala ya kiuongozi, kielimu, na kubaguliwa katika kufanya baadhi ya kazi muhimu. Pia walinyimwa uhuru wa kumiliki mali zao binafsi. Walitakiwa kukaa nyumbani huku wakiwafulia nguo waume zao, wakiwapikia chakula waume zao, na kulea watoto.

Ikawa kila siku Mzee Makunganya alipokuwa anakwenda kunywa pombe na wazee wenzake, huwa wakimdhihaki kwa kumwambia; “Inawezekanaje hadi anafikia umri alionao hana mtoto wa kiume?”

Ndipo siku moja Mzee Makunganya alipohamaki na kuanza kumtusi Mzee majivuno. Wazee wengine waliingilia kati ugomvi huo ulioanzishwa na Mzee Majivuno. Baada ya kupatanishwa, kila mmoja alishika hamsini zake.

Mzee Makunganya alipofika nyumbani kwake, alimkuta mkewe pamoja na binti zake wakiwa wanakula chakula cha usiku. Kabla ya salamu, alimshika mkewe na kuanza kumpiga huku akisema; “Kwanini haujanizalia mtoto wa kiume?”

Akiwa anaendelea kumpiga mkewe, kati ya wale binti zake mmoja aliyeitwa Akilinyingi ambaye ndiye kifungua mimba, aliingilia ugomvi huo na kuanza kumuokoa mama yao. Akimuuliza baba yake;

“Baba, kwanini kila siku huwa unampiga mama? Kwani hujui kupata mtoto wa kiume ni mipango ya Mungu? Kwa hiyo acha kumpiga mama na tuendelee kumuomba Muumba ili siku moja na sisi tumpate kaka yetu.”

Mzee kusikia maneno ya mwanawe, akaacha kumpiga mkewe kisha akaingia ndani na kujifungia chumbani. Akilinyingi akamwita mdogo wake Adili, kisha wakamfuata mama yao aliyelala chini akilia. Wakamnyanyua na kumkalisha kwenye kiti huku Akilinyingi akisema;

“Katika kijiji chetu cha Patapata uonevu na manyanyaso yamezidi kwa wabeba wana hivyo ni lazima tutafute namna ya kujikomboa. Adili naye akaongezea kwa kusema, “tunatakiwa tufanye mkutano ili tuweze kung’amua njia kabambe ambazo zitaweza kutumika kukomesha kabisa tabia mbaya ya manyanyaso na machukizo kwetu sisi wabeba wana.”

Walipomaliza maongezi wote waliingia vyumbani kulala. Kesho yake asubuhi jua lilipokuwa linaanza kuwia, ilisikika sauti ikisema;

*“La mgambo likilia, lina jambo! Wasikie wapatapata.*
*Mashakani tuondoke, wabeba wana maendeleo wajipatie.*
*La mgambo, likilia lina jambo!*”

*Wapatapata kusikia mbiu, furaha waliipata.*
*Wabeba wana vitanda havikuwashika,*
*Wana migongo nao mbio wakienda mkutanoni.*

Akilinyingi, Adili pamoja na mama yao, walikwenda pia. Baada ya wabeba wana wote kukusanyika, Akilinyingi binti mkubwa wa Mzee Makunganya alisimama na kusema, “Wabeba wana wa Patapata oyeeeeee!” Akaendelea kuongea kwa kusema, ‘imepita miaka mingi tangu enzi za mababu wa mababu zetu, sisi wabeba wana tukinyanyaswa na kubaguliwa katika kila jambo wakati uwezo wa kufanya mambo ya kujipatia maendeleo yetu binafsi tunao. Leo tumekusanyika mahali hapa ili tutafute mwafaka wa mbinu sahihi za kuzitumia ili na sisi tushike hatamu katika masuala ya kiuongozi na hata katika kushiriki kwenye shughuli za uvunaji wa munyu.

Mama Maneno alisimama na kudakia maongezi kwa kusema, “kweli kabisa kule kwenye uvunaji wa munyu, ile kazi tunayoifanya ni sawasawa na *nunge*. Tunafanya kwa kuwa wahenga husema, “mkaa bure si sawa na mtembea bure, labda huenda akaokota. Kwa hiyo mwaka huu lazima tuwaonyeshe akina baba kuwa sisi ni akina nani!”

Wabeba wana wote walishangilia kwa vifijo, vigelegele, na nderemo. Hapo ndipo mke wa Mzee Makunganya aliposimama huku akilia kisha akaanza kwa kusema, “jamani mimi mwenzenu mume wangu hunipiga kila siku eti kwa sababu sina mtoto wa kiume. Pia kila ninapoenda kuvuna munyu, huninyang’anya ujira wangu kisha kwenda kununulia *mataputapu*.” Mama Maneno aliingilia kati na kusema; “Sasa unalia nini? Tumeitana hapa ili tutafute mwafaka wa hayo manyanyaso yanayotukabili.”

Kulipita kimya kitambo kisha Akilinyingi alisimama tena kwa kujiamini na uthubutu wa kutosha! Kilipita kimya tena bila kutia neno watu wakimwangalia na kumsikiliza kwa makini kisha akaendelea, “mwaka huu lazima niingie kwenye kinyang’anyiro cha kuwania uongozi katika uchaguzi wa serikali za mitaa nafasi ya Mwenyekiti wa kijiji hiki cha Patapata.”

Wabeba wana wote walisimama wima! Wakushangilia, walishangilia! Wakupiga vigelegele, walipiga vigelegele! Kisha baada ya muda kupita, wote walikaa kimya na kutega masikio yao. Akilinyingi aliongeza kwa kusema tena, “mtanichagua kuwa Mwenyekiti wa kijiji hiki cha Patapata?” Kama kawaida yake Mama Maneno alidakia kwa kusema; Umeshapata! Watu wote walicheka halafu Akilinyingi akaendelea kwa kusema kwamba, ‘nitahakikisha na sisi wabeba wana tunashika hatamu kwenye kamati za uongozi wa kijiji. Pia nitahakikisha wabeba wana na akina baba wanakuwa sawa kwenye uvunaji munyu, wabeba wana watapata chao kilicho halali bila dhuluma ya aina yoyote, na nitazuia uonevu na manyanyaso juu ya wabeba wana.”

 © 2022

Mama maneno ambaye kwenye mkutano huo alichukua nafasi ya Mwenyekiti, alisimama na kufunga mkutano kwa kusema, “mgaagaa na upwa hali wali mkavu.” Akiwa na imani kuwa siku moja yataonekana matunda ya mahangaiko yao.

Jua lilipokuchwa na mkutano wa wabeba wana ndipo ulipofungwa na wote wakawa wanarudi makwao wakiwa wamefurikwa na furaha mioyoni mwao.

Taarifa ya kuwa wanawake nao wanataka kugombea nafasi za uongozi wa kijiji zilisambaa na kuwafikia akina baba. Uamuzi wa wanaume wa Patapata ukawa ni kwenda kuwatishia wake pamoja na binti zao, miongoni mwa wanaume hao alikuwemo Mzee Makunganya. Alipofika nyumbani kwake jambo la kwanza alimwita mkewe pamoja na binti zake na kusema, “sitaki kusikia eti kuna mmoja kati yenu anataka kuwa kiongozi katika kijiji hiki cha Patapata. Nikija kusikia, nitampiga mtu huyo hadi ajute kuzaliwa.” Akaongezea akisema, ‘ninyi wabeba wana hamna haki ya kuwa viongozi katika kijiji hiki.”

Siku za uchaguzi wa viongozi wa serikali za mitaa nchi nzima ziliwadia. Wabeba wana wa kijijii cha Patapata walimpendekeza Akilinyingi binti wa Mzee Makunganya awe mgombea wa nafasi ya Uenyekiti akishindishanishwa na Mzee Maneno, mume wa Mama Maneno.

Siku ya uchaguzi ilipotimu, wazee kwa vijana walikusanyika kwenye eneo linalotumika kufanyia uchaguzi. Baada ya zoezi la upigaji kura kukamilika na kura zote kuhesabiwa. Ulifika muda wa kutangaza matokeo.

Mtoa matangazo alichukua kipaza sauti na kusema, “Wapatapata oyeeeee!” Watu wote waliitikia kwa pamoja oyeeee! Halafu wakakaa kimya. Baada ya muda mtangazaji akasema tena, wabeba wana wa Patapata oyeeeee! Nao hawakubaki nyuma, waliitikia oyeee! Akaendelea kwa kusema, kutokana na matokeo ya kura zilizopigwa mwaka huu, aliyeshinda niiiiii…….! Akakaa kimya kidogo halafu akamalizia akisema ni Akilinyingiiiii! Bila kuchelewa wabeba wana waliinuka huku wakishangilia kama wamepandwa na wazimu wakiachwa akina baba wasiamini kilichotokea.

Baada ya matokeo hayo yaliyomtangaza Akilinyingi kuwa mshindi, alisimama na kusema, “sisi wabeba wana tukiamua kufanya jambo, hakuna tulishindwalo. Nashukuru kwa kuniamini. Nawaahidi kupitia kamati za serikali ya kijiji, nikishirikiana na wajumbe wote kwa maana ya wake kwa waume tutafikia malengo.”

Siku ile ikaisha huku Akilinyingi akiwa ndiye mshindi wa uchaguzi uliofanyika. Alipofika nyumbani kwao alimkuta baba yake akiwa na hasira mithili ya mbogo. Alisema; “kwanini umenidhalilisha kiasi hiki? Kwani hujui kwamba wewe ni mtoto wa kike?” *Alisikika akiuliza baba yake Akilinyingi*.

Ndipo Adili ambaye ni binti mdogo wa Mzee Makunganya alipomuuliza baba yake, “kwani baba huna furaha kwa binti yako kuwa Mwenyekiti wa kwanza wa kike katika kijiji cha Patapata?” Mzee Makunganya alitafakari maneno ya binti yake kwa muda, kisha akacheka na kusema, “kweli wanangu mmefanya jambo la maana.” Kisha akawakumbutia binti zake wote wawili akiwa na furaha tele.

Mawio ya siku inayofuata, kamati ya wajumbe pamoja na wabeba wana wengine walimfuata Akilinyingi hadi nyumbani kwao akiwemo mama Maneno. Wote walikaribishwa na baada ya kuketi kwenye jamvi, ndipo Mama Maneno alipoanza kwa kusema, “Mwenyekiti lazima tupange mpango kabambe juu ya suala la usawa.” Baada ya mazungumzo, Akilinyingi alifunga kikao kwa kusema ataitisha mkutano wa wanakijijii wote ili wazungumze kwa pamoja.

Muda uliopangwa ulipofika, la mgambo lililia kuitisha mkutano wa wanakijiji wote wa Patapata. Wabeba wana, wana migongo pamoja na akina baba wote walitimua mbio kuelekea mkutanoni.

Watu wote walipofika, Mwenyekiti mpya ambaye ni Akilinyingi alichukua nafasi ili kufungua mkutano kwa kusema, "Wanakijiji wa Patapata oyeeee!" Wote waliitikia, oyeee! *Basi Mwenyekiti akaendelea kusema*; 'kuanzia sasa wabeba wana na akina baba wote ni sawa sio kwenye kumiliki mali binafsi na wala sio kwenye migodi ya munyu pekee, yaani kila mahali na hata kwenye masuala ya uongozi na kazi zote zitafanywa kwa usawa bila ya ubaguzi wa aina yeyote ile! Uwe wa kijinsia na hata kiutajiri!"

Basi wabeba wana kusikia maneno yale walishangilia bila kifani huku akina baba macho yakiwatoka kwa hasira wasijue nini cha kufanya. Akamaliza kwa kusema, "kwa yeyote atakayepingana na sheria zilizowekwa, hatua kali itachukuliwa dhidi yake ikiwemo kufukuzwa katika kijijii hiki." Basi mkutano uliishia hapo na watu wote walitawanyika kurudi nyumbani.

Sifa za Akilinyingi na uongozi wake zilisambaa pande zote za dunia. Tangu siku ile, amani, furaha, upendo, haki, pamoja na usawa ukatawala katika kijiji cha Patapata

Hivyo ndivyo watu wa Patapata walivyopata utawala bora wa mwanamke aliyepatikana ndani ya kijiji cha Patapata.

**Mtunzi: OMARY HASSAN MAKUNGANYA**
**Shule**: MTWARA TECH SECONDARY SCHOOL
**Kidato**: FORM THREE – CIVIL ENGINEERING
**Wilaya**: MTWARA , **Mkoa**: MTWARA

## 6.2 HADITHI YA MSHINDI WA PILI

Hadithi hadithi!
Hapo zamani za kale kulikuwapo kijiji kimoja kilichojulikana kwa jina la Wapendanao. Kijiji hicho kilikuwa na sifa kama jina lake kwa maana, watu wa rika na jinsi tofauti waliweza kupendana na kushirikiana katika kila jambo. Walitambua kuwa *umoja ni nguvu, utengano ni udhaifu*. Ingawa licha ya upendo huo, wanakijiji waliishi kwa kufuata mila na desturi za zamani ambazo wanawake walikosa haki ya kupata elimu. Hawakujua kama *avumaye baharini ni papa kumbe wengi wapo*. Waliamini wavulana pekee ndiyo waliokuwa na haki ya kupata elimu na kuwa na akili nyingi kuliko wasichana.

 © 2022




Katika kijiji hicho kulikuwa na familia moja ya mzee maarufu aliyeitwa Mzee Mpemba. Mzee huyo alibahatika kupata watoto watatu ambao ni Hassan, Hussein, na Samia. Kama desturi, Samia alikuwa anabaki nyumbani kumsaidia mama yake kazi za nyumbani wakati kaka zake wakiwa shuleni.

Licha ya Samia kutokwenda shule, alikuwa na shauku kubwa ya kutaka kujua kile kakaze wanachojifunza wakiwa shuleni. Pindi warudipo kutoka shuleni, Samia **alisaili** walichosoma. Alionesha jitihada za kujifunza kwani *ukitaka uzuri sharti uzurike.* Kaka zake hawakuweza kumkatalia mdogo wao, walianza kumfundisha mambo machache ili na yeye asiwe nyuma kielimu japokuwa ilikuwa si rahisi kwake kuelewa kwa haraka. Lakini *iwapo nia njia hupatikana*, waliamini mdogo wao ataweza. Muda sio mrefu akaweza kujua mawili matatu lakini alizidi kupambana ili aongeze ujuzi sababu alivutiwa na elimu. Ama kweli *anayechonga mzinga ameionja asali.*

Siku moja Samia aliagizwa na mama yake sokoni akanunue vyombo vya jikoni. Ila katika pitapita zake aliweza kukutana na mzee mmoja aliyekuwa anauza magazeti. Samia alisogea karibu na meza kwa taadhima hadi pale yalipokuwa magazeti na kuanza kupekua gazeti moja hadi jingine.



Katika pekua pekua aliweza kukutana na habari iliyohusu utoaji wa ajira kwa wasichana wanaojua kusoma na kuandika. Samia alifurahishwa sana na habari hiyo kwani *kila mwamba ngoma, ngozi huvutia kwake.*

Baada ya kusoma tangazo, alielekea sokoni kununua mahitaji kama alivyoagizwa na mamaye. Aliporudi nyumbani aliwataarifu kaka zake kuwa ana jambo zuri analohitaji kuwashirikisha. Vijana walifurahia taarifa hiyo waIijua kuwa mdogo wao amepata taarifa nzuri.


Baada ya kumaliza shughuli zake ndipo alipowaambia alichokiona gazetini. Kaka zake walijua kuwa *hayawi hayawi yamekuwa.* Walimpa moyo mdogo wao na kuamua kwenda kuwataarifu wazazi wao.

Hakika haikuwa kazi rahisi kwa wazazi hao kukubaliana na kile walichoambiwa na watoto wao lakini waliamini kuwa *alipangalo Mungu hamna anayeweza kulipangua* ama kutolifanikisha. Ndipo mwishowe wazazi waliweza kukubaliana na uamuzi wa Samia wa kwenda kufanyiwa usaili.

Siku iliyofuata Samia na **ghulamu** Hussein walifunga safari kuelekea mjini ambako kazi hiyo iliweza kutangazwa. Samia alikuwa na hofu sana kwa sababu ilikuwa ni mara yake ya kwanza kusafiri kwenda mjini lakini aliondoa shaka kwa kusema *kiingiacho mjini si haramu*.

Njiani samia alishangazwa sana na mazingira ya mjini. Aliweza kuona barabara nzuri za kuvutia pamoja na majengo mbali mbali kitu ambacho kilimstaajabisha. Pia aliona wasichana kwa wavulana wakielekea shuleni pia akaona wanawake watatu walivalia gwanda za jeshi wamesimama barabarani, alistaajabishwa sana na jambo hilo.

 © 2022




Samia alijua wasichana kazi zao ni zile za nyumbani kama ilivyo kijijini kwao. Alimuuliza kaka yake kuhusu suala hilo, kaka yake aliweza kumwambia kwamba huku kuna kitu kiitwacho serikali. Serikali inahusika na kulinda haki za watu wote wasichana kwa wavulana. Samia hakuweza ridhika na ufupi wa jibu alilopewa na kujiahidi kulifuatilia.

Baada ya samia kushinda usaili uliofanyika sehemu ya utoaji wa ajira iliyotangazwa, alifanikiwa kupata kazi. Akiwa anaendelea kufanyakazi za ndani kwa mwajiri wake, alipata muda wa kufuatilia suala la serikali inayolinda haki za raia kama alivyojiahidi. Alijua vitu vingi vizuri ambavyo serikali inavifanya ambavyo vinamfanya mtu yeyote kuwa huru katika kila jambo kwa mujibu wa sheria awe msichana au mvulana.

Samia alipendezwa sana na utendaji kazi wa serikali akiamini kuwa serikali ni kama madini yanayoweza kumpa msichana thamani anayostahili maishani.

Baada ya siku nyingi kupita, samia aliweza kurudi kijijini kwao. Yeye pamoja na kaka yake Hussein walianza kutoa elimu juu ya suala zima la haki za binadamu. Elimu hiyo akaweza kuwaheshimisha wasichana wenzake na wao wakawa chachu ya maendeleo katika jamii na nchi kwa ujumla.

**Mtunzi:** HUSSEIN ABDALLAH HUSSEIN
**Shule:** SHULE YA SEKONDARI – MTWARA UFUNDI.
**Kidato:** KIDATO CHA NNE – MITAMBO
**Wilaya**: MTWARA
**Mkoa**: MTWARA

## 6.3 HADITHI YA MSHINDI WA TATU

“Wanawake wanaweza katika shughuli mbalimbali za kujiendeleza kiuchumi. Hivyo hatutaraji kuona mwanamke yeyote akikata tamaa katika mambo mbalimbali ya kiuchumi. Kwani mwanamke ni nguzo katika familia na hata jamii mzima. Kwa ujumla mwanamke anaweza kufanya shughuli yeyote ambayo italeta kipato kwenye jamii kama vile ujenzi na uchimbaji wa madini. Pia hatuoni sababu ya mwanamke kubakia nyuma kimaendeleo maana haki zao zote wanazipata.”

Mfano; kulikuwa na mama mmoja aliyeitwa Amina. Mama huyo alikuwa na watoto watatu ambao ni John, Imani, na Amana. Mume wa Amina yaani baba wa watoto hao watatu aliaga dunia wakati watoto wao wakiwa na umri mdogo. John alikuwa anasoma darasa la nne wakati Imani na Amana walikuwa wanasoma darasa la pili.

Baada ya miaka mitatu kupita, John alihitimu Elimu ya Msingi. Wakati huo mama yake Bi. Amina hakuwa na fedha za kumpeleka mwanae kujiunga na kidato cha kwanza.

John alipoona hapelekwi shuleni, aliamua kwenda kuomba ajira migodini. Aliishi huko miezi kadhaa bila kupata fedha za kutosha zaidi ya vihela kidogo vilivyomwezesha kuendelea kuishi. Aliamua kurudi nyumbani kuungana na familia yake.

John alimkuta mama yake Bi. Amina anaendelea kupambana ili kupata fedha za kujikimu pamoja na za kulipia gharama za mahitaji ya shule ya watoto wake wawili waliobakia nyumbani. Hivyo nae aliunganishwa nao, nae alirudishwa shuleni kuendelea na masomo.

Bi. Amina alijitahidi kadri ya uwezo wake kuhakikisha watoto wake wanapata elimu bora na si bora elimu. Watoto walisoma kwa bidii sana na baada ya miaka kadhaa kupita, John alifanikiwa kupata ajira ya Ualimu. Kuanzia hapo maisha yao yalipata nafuu na furaha kwa sababu John alimsaidia mama yake kusomesha wadogo zake.

Na wale watoto wawili ambao ni Imani na Amana walimaliza masomo ndipo Imani akawa Mwanasheria na Amana akawa Daktari wa binadamu. Bi. Amina alifurahi sana kuona watoto wake wametimiza ndoto zao.

**Mtunzi:** HAWA SALUMU MGAYA
**Shule:** SHULE YA SEKONDARI NASULI
**Kidato:** KIDATO CHA KWANZA
**Wilaya:** NAMTUMBO
**Mkoa**: RUVUMA





## 6. 4 HADITHI YA MSHINDI KATI YA WASHINDI KUMI (10)

Kulikuwepo binti mmoja aitwaye Rehema aliyekuwa anaishi mtaa wa Chuno katika manispaa ya Mtwara Mikindani. Aliikuwa ni binti mwenye umri wa miaka kumi na nane ambaye hakupata fursa ya kupelekwa shule tangu akiwa na umri mdogo. Hali hiyo ilitokana na maisha duni waliyokuwa nayo wazazi wake.

Siku moja binti huyo alikutana na kijana mmoja aliyejitambulisha kuwa anaitwa Nasri, ambaye alikuwa kwenye mafunzo ya Udaktari katika hospitali ya mkoa wa Mtwara – Ligula na kupelekea kuwa wapenzi.

Baada ya mafunzo kwisha, Nasri aliondoka bila kumuaga mpenzi wake Rehema. Siku chache zilipita Rehema akagundulika ana *"kitumbo"* na alipowaza *"kuichomoa"* wazazi wake walimkataza. Ndipo baada ya miezi tisa, alijifungua watoto mapacha.

Baada ya siku kadhaa kupita, Rehema aliamua kujishughulisha katika kazi mbalimbali ili aweze kulisha watoto wake pamoja na kuwasomesha ili isiwe kama ilivyokuwa kwake. Kwa kutopelekwa shule kutokana na uhaba wa fedha.

Kazi aliyoipata kwa haraka ilikuwa ni kugonga kokoto katika eneo fulani liitwalo Tangita huko Mbae Mtwara. Lakini hakuishia hapo, aliamua kuhama mji na kwenda mbali kidogo na mji wa Mtwara. Alikwenda Nachingwea Lindi kuchimba madini.

Watu wengi walimshangaa kwa uamuzi wake lakini hakujali, aliendelea kupambana mpaka alipofanikiwa kupata madini. Baada ya kuuza madini na kupata fedha, aliamua kurudi nyumbani kwao ili ailinde familia yake.

Hatimaye Rehema alirudi Mtwara kwa furaha kubwa na aliweza kuwasomesha watoto wake, kujenga nyumba huko Mangamba karibu na Shule ya Sekondari ya wasichana ya Mtwara. Pia alifungua hoteli iitwayo Shikamo madini iliyopo Masasi.

Basi Rehema aliweza *"kutoboa"* maisha yake kupitia madini na aliishi maisha ya furaha daima, yeye pamoja na familia yake.

**Mtunzi:** SABRINA AMANI MALUZUKU
**Shule:** SHULE YA SEKONDARI MTAPIKA
**Kidato:** KIDATO CHA NNE
**Wilaya:** MASASI
**Mkoa:** MTWARA

## 6.5 ZAWADI

Mshindi wa kwanza; Cheti pamoja na fedha taslimu Tsh. 100,000/=
Mshindi wa pili; cheti pamoja na fedha taslimu Tsh. 70,000/=
Mshind wa tatu; cheti pamoja na fedha taslimu Tsh. 60,000/=
Mshindi wa nne; cheti pamoja na fedha taslimu Tsh. 40,000/=
Washindi wengine @ Tsh. 20,000/=

 © 2022

Imeandaliwa na;
**MWANAWETU MMUNI**

# MWANAWETU BOOKS AND CONSULTANCY

**©MWANAWETUBOOKS 2022**